Nuru ya Kiswahili, Juzuu 5(1), Juni 2026:47-67
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru51.4767

# Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Pili katika Shule za Upili nchini Rwanda: Mifano kutoka Shule Teule Wilayani Musanze

**Faustin Ndikubwimana**
**Mhadhiri Msaidizi, Rwanda Polytechnic-Kigali College**
ndikubwimanafaustin@gmail.com

## Ikisiri

Makala inajadili mikakati inayotumiwa na walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili katika shule teule za sekondari wilayani Musanze, nchini Rwanda. Licha ya jitihada za serikali za kukiendeleza Kiswahili tangu kutambuliwa kwake kama lugha rasmi mwaka 2017, ufundishaji wake bado unakabiliwa na changamoto mbalimbali, zikiwemo uhaba wa vifaa vya kielimu na walimu wenye weledi, mtazamo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili, na kutokuwepo kwake katika mitihani ya taifa kwa ngazi ya chini ya sekondari. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Viwezeshi ya Gibson (1977). Mtafiti alitumia mbinu za ushuhudiaji na usaili, huku walengwa wakiwa walimu wa Kiswahili na wanafunzi kutoka Groupe Scolaire (G.S.) Muhoza I na Ecole de Sciences de Musanze (E.S.M.). Matokeo yalibaini mikakati mitano. Nayo ni: kuboresha makundi ya kujifunza ili kukabiliana na uhaba wa vitabu na kamusi, kuimarisha ushirikiano baina ya walimu kupitia mitandao ya kijamii, kutumia simu za mkononi kama teknolojia mbadala ya kufundishia, kuandaa mashindano na mijadala ya Kiswahili ili kujenga ujasiri wa kuongea, na kuhamasisha wanafunzi kuhusu umuhimu wa Kiswahili katika fursa za ajira na biashara. Matokeo yanathibitisha kuwa ingawa viwezeshi vya kimwili ni vichache, walimu wamefanikiwa kutumia viwezeshi vya kijamii na kisaikolojia kukabiliana na changamoto hizo.

**Dhana za Msingi:** Lugha ya pili, ufundishaji, ujifunzaji, mikakati, nadharia ya viwezeshi

## Utangulizi

Lugha ya Kiswahili ni mojawapo ya lugha zinazokua kwa kasi duniani katika nyanja ya ufundishaji wa lugha ya pili. Mbinu za ufundishaji wa lugha hii hubadilika mara kwa mara ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na mabadiliko ya kiteknolojia (Zhong, 2024). Lugha ya Kiswahili inachukua nafasi muhimu katika elimu ya lugha ya pili kwa kuwa watu wa kutoka mataifa mbalimbali duniani wanajifunza. Baadhi ya nchi zinazojitokeza katika kufundisha Kiswahili kama lugha ya pili ni Uingereza, Ujerumani, Japani, Marekani, pamoja na nchi za Afrika Mashariki na Kati (Saleh, 2019).

Nchini Rwanda, Kiswahili kinatumika kama somo la pili. Ujifunzaji wake unaweza kuongeza fursa za ajira, biashara za kimataifa, elimu ya juu, na kuboresha maisha ya mtumiaji (Crystal, 1997). Hivyo, lugha ya Kiswahili haiishii tu kuhudumia kama chombo cha mawasiliano, bali pia inakuza maendeleo ya kiuchumi, kibiashara, kisiasa, na kielimu. Aidha, ufundishaji wa Kiswahili unachukuliwa kuwa muhimu kwa kuwa unaimarisha mawasiliano ya kikanda na diplomasia (Niyomugabo, 2016).

Ufundishaji wa Kiswahili nchini Rwanda unaweza kugawanywa katika vipindi viwili vikuu ambavyo ni kipindi cha ukoloni na kipindi baada ya uhuru. Kipindi cha ukoloni kilijumuisha utawala wa Kijerumani na Ubelgiji (Mlaga, 2017). Wakati wa utawala wa Kijerumani, ufundishaji wa Kiswahili ulianza mwaka 1907 (Ntawiyanga, 2020). Hata hivyo, kufuatia kushindwa kwa Wajerumani katika Vita vya Kwanza vya Dunia, wakoloni wa Kibelgiji walipokelewa Rwanda na walitumia Kiswahili kama lugha ya wahalifu, huku Kifaransa kikipata nafasi ya kuwa lugha rasmi.

Kipindi baada ya uhuru kilianzia mwaka 1979, ambapo serikali ya Rwanda ilichukua hatua za kukuza Kiswahili kwa kushirikiana na Tanzania kupitia mpango wa kubadilishana walimu (Mlaga, 2017). Mpango huu ulitekelezwa mwaka 1979 wakati somo la Kiswahili likiwa na saa nne za kufundisha kwa kila wiki. Aidha, kuanzia mwaka 2008 hadi sasa, Kiswahili kinafundishwa kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha tatu, huku shule za ngazi ya juu zikitoa Kiswahili kama chaguo la hiari katika michepuo isiyo ya lugha (Mlaga, 2017).

Licha ya jitihada zilizofanywa, ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili bado unakabiliwa na changamoto mbalimbali, zikiwamo upungufu wa walimu wenye ujuzi, ukosefu wa vifaa vya kielimu, na kutokuwa na mtaala unaoruhusu ujifunzaji endelevu. REB (2015) inaonesha kwamba Kiswahili kimejumuishwa katika mtaala wa shule za upili kuanzia kidato cha kwanza hadi cha tatu, lakini hakiorodheshwi katika masomo ya kitaifa kwa ngazi ya chini. Jambo hili linapunguza ufanisi wa ujifunzaji na kuathiri uelewa wa lugha. Matokeo yake, baadhi ya wanafunzi hushindwa kutumia Kiswahili kikamilifu katika mawasiliano ya kila siku; hivyo hupunguza nafasi za kitaaluma na kiuchumi zinazotokana na umiliki wa lugha ya pili (REB, 2015; Mlaga, 2017).

Tangu Kiswahili kitambuliwe kama lugha rasmi mwaka 2017, serikali imeendelea kukiendeleza kupitia mtaala wa umahiri. Mtaala huu unalenga kukuza stadi za mawasiliano na matumizi ya lugha katika miktadha halisi ya kijamii na kiuchumi (REB, 2015). Katika muktadha huu, watafiti wameelekeza mjadala wao kwenye mikakati inayoweza kuboresha ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili, wakisisitiza umuhimu wa

malengo ya lugha kama mwongozo wa mbinu, nyenzo, na tathmini darasani.

Kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali kama vile Rivers (1981) na Dörnyei (2001), mikakati inayotumika katika ufundishaji wa lugha ya pili inapaswa kuzingatia ushirikishwaji wa wanafunzi. Wanaongeza kuwa mbinu shirikishi kama vile majadiliano, michezo ya maneno, usimulizi wa hadithi, na kazi za makundi huongeza ushiriki wa wanafunzi na kuimarisha uelewa wa lugha. Aidha, Cary (2000) anasisitiza umuhimu wa kupunguza usemaji wa mwalimu darasani. Hatua hii inawapa wanafunzi nafasi ya kujieleza na kujenga kujiamini katika matumizi ya lugha. Mikakati hii inaonesha kuwa ujifunzaji wa lugha ni mchakato wa kijamii unaohitaji mazingira wezeshi na mwingiliano endelevu.

Vilevile, tafiti zinaonesha kuwa motisha ni nguzo muhimu katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Jarvis (2005), Harrison (2004) na Maina (2003) wanabainisha kuwa motisha huimarika pale wanafunzi wanapopata maoni chanya, kushirikishwa katika shughuli za darasani, na kuhisi kuwa lugha wanayojifunza ina thamani katika maisha yao ya sasa na ya baadaye. Sambamba na hilo, Mbito (2013) anapendekeza uwepo wa sera za lugha shuleni. Kwa mfano, siku maalumu za kuzungumza Kiswahili zinaweza kuongeza matumizi ya lugha nje ya darasa na kuifanya iwe sehemu ya maisha ya kila siku ya mwanafunzi.

Aidha, kukuza utamaduni wa kusoma vitabu vya Kiswahili ni muhimu. Matumizi ya nyenzo za ziada kama vilabu vya lugha, mashindano ya shule, na maabara za lugha yameonekana kuongeza msamiati, uelewa, na ufasaha wa wanafunzi (Gathumbi na Masembe, 2005; Yang, 2008).

Niyomugabo (2016) anaongeza kuwa matumizi ya teknolojia kama vile redio, runinga na tarakilishi husaidia wanafunzi kuwasiliana na lugha hata nje ya mazingira ya darasa, jambo linalochangia ujifunzaji endelevu.

Hata hivyo, maandiko yanaonesha kuwa utekelezaji wa mikakati hii hauko sawa katika shule zote. Changamoto kama vile upungufu wa walimu wenye ujuzi wa kufundisha Kiswahili kama lugha ya pili, ukosefu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, pamoja na nafasi ndogo ya Kiswahili katika tathmini za kitaifa huathiri ufanisi wa mikakati iliyopendekezwa (REB, 2015; Mlaga, 2017). Vilevile, Akaka (2017) na Oloo (2018) wanaonesha kuwa, licha ya walimu kupendekeza na kutumia mikakati shirikishi kama uundaji wa makundi ya wanafunzi, utekelezaji wake hukwamishwa na uhaba wa rasilimali na mazingira yasiyo wezeshi. Hali hii inaashiria pengo kati ya mikakati inayopendekezwa kitaaluma na utekelezaji wake katika mazingira halisi ya shule.

Kwa kuwa changamoto hizi zinaathiri malengo ya elimu ya sekondari nchini Rwanda, kuchunguza mikakati inayotumika katika shule teule wilayani Musanze ni muhimu. Uchunguzi huu utasaidia kuongeza ufanisi wa ujifunzaji na kuhakikisha kuwa ujifunzaji wa Kiswahili unakidhi mahitaji ya kikanda na kimataifa. Makala hii inajitofautisha na tafiti zilizotangulia kwa kufafanua mikakati inayotumika kwa vitendo katika shule teule wilayani Musanze, badala ya kujikita tu katika changamoto au mapendekezo ya jumla. Makala inabainisha jinsi walimu na shule zinavyotekeleza mikakati hiyo katika muktadha wao halisi, ufanisi wake, na mchango wake katika kuboresha ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Kwa kufanya hivyo, makala hii inalenga kuchangia maarifa mapya

yanayoweza kusaidia sera, mafunzo ya walimu, na uboreshaji wa ufundishaji wa Kiswahili nchini Rwanda.

**Nadharia ya Utafiti**

Nadharia ya Viwezeshi (*Affordance Theory*) iliyoanzishwa na James Jerome Gibson (1977, 1979) ndiyo iliyoongoza mjadala wa matokeo ya utafiti huu. Gibson alikuwa mwanasaikolojia wa Kimarekani aliyebobea katika mtazamo wa kiikolojia kuhusu utambuzi wa binadamu. Nadharia hii inasisitiza kwamba mafanikio ya ujifunzaji wa lugha ya pili yanategemea uwezo wa mwanafunzi, mazingira yanayomzunguka mwanafunzi, pamoja na jinsi mazingira hayo yanavyomwezesha au kumzuia kujifunza (Gibson, 1977). Mawazo makuu ya nadharia hii, kama asemavyo Gibson (1979), viwezeshi ni vitu vinavyotoa uwezekano wa vitendo ambavyo mtumiaji anaweza kuchukua kutokana na hali fulani; kwa maneno mengine, ni namna ambavyo mazingira yanavyomruhusu mtu kufanya au kushindwa kufanya jambo fulani. Nadharia hii imekuwa ikiungwa mkono na wataalamu mbalimbali katika uga wa elimu. Ndikubwimana (2023) alitumia nadharia hii katika kufafanua changamoto za ufundishaji wa Kiswahili nchini Rwanda, akibainisha kwamba ushirikiano kati ya walimu, wanafunzi, na wazungumzaji wa asili wa lugha ni kiwezeshi muhimu katika ujifunzaji wa lugha ya pili.

Nadharia ya Viwezeshi ina mihimili minne katika muktadha wa ujifunzaji wa lugha. Mhimili wa kwanza unahusu viwezeshi vya kimwili ambavyo ni miundombinu, vitabu, kamusi, maabara ya lugha, teknolojia, na vifaa vingine vya kielimu. Mhimili wa pili unahusu viwezeshi vya kijamii kama vile mwingiliano kati ya walimu na wanafunzi, ushirikiano, mawasiliano ya kila siku, na uhusiano wa kijamii. Mhimili wa tatu unahusu viwezeshi vya

kitaaluma vinavyojumuisha mtaala, mbinu za ufundishaji, tathmini, na ujuzi wa walimu. Mhimili wa nne unahusu viwezeshi vya kisaikolojia kama motisha, mtazamo, kujiamini, na hisia za wanafunzi kuelekea lugha.

Katika utafiti uliozalisha makala hii pamoja na mjadala wa makala hii, mihimili yote minne imetumika. Mhimili wa viwezeshi vya kimwili umetumika kuchunguza upatikanaji wa vitabu, kamusi, na vifaa vya teknolojia katika shule teule. Mhimili wa viwezeshi vya kijamii umetumika kutathmini ushirikiano baina ya walimu na wanafunzi. Mhimili wa viwezeshi vya kitaaluma umesaidia kubainisha mbinu za ufundishaji zinazotumika. Mhimili wa viwezeshi vya kisaikolojia umetumika kuchunguza motisha na uhamasishaji wa wanafunzi. Sababu ya kutumia mihimili yote minne ni kwamba ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili ni mchakato unaohusisha nyanja zote hizo kwa pamoja; hivyo, kama ungetumika mhimili mmoja au baadhi ya hiyo nminne kungeweza kutoa picha isiyokamilika ya hali halisi. Kwa ujumla, nadharia ya Viwezeshi ilitupa msingi thabiti wa kimuundo wa utafiti, kuruhusu kuchambua jinsi mazingira ya shule, walimu, na vifaa vinavyosaidia au kuzuia ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili nchini Rwanda.

## Methodolojia ya Utafiti

Makala hii ilitumia mkabala wa kitaamuli ili kuchunguza mikakati inayotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Kwa kuzingatia kuwa ujifunzaji wa lugha huhusisha mwingiliano wa kijamii na mazingira ya darasa, mkabala huu uliwezesha kupata uelewa wa kina kuhusu mbinu za ufundishaji, ushiriki wa wanafunzi, na matumizi ya lugha katika hali halisi.

Kuhusu eneo la utafiti, utafiti uliozalisha makala hii ulihusisha shule mbili za sekondari wilayani Musanze, ambazo ni Groupe Scolaire Muhoza I na École des Sciences de Musanze. Shule hizi ziliteuliwa kwa makusudi kwa sababu zinafundisha Kiswahili katika ngazi ya chini ya sekondari. Vilevile, utafiti ulijumuisha walimu wa Kiswahili na wanafunzi wa kidato cha pili na cha tatu, ambao ndio walengwa wakuu wa utekelezaji wa mikakati ya ufundishaji wa lugha ya pili.

Kwa upande wa ukusanyaji wa data, mbinu ya ushuhudiaji ilitumika ili kupata taarifa za moja kwa moja kuhusu mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani. Katika muktadha huo, mtafiti alihudhuria vipindi vya Kiswahili katika madarasa ya kidato cha pili A na kidato cha tatu A na B, ambapo alichunguza mbinu za ufundishaji, kiwango cha ushiriki wa wanafunzi, na namna mikakati mbalimbali inavyotekelezwa. Zaidi ya hayo, usaili ulifanywa na walimu watatu wa Kiswahili pamoja na wanafunzi tisa walioteuliwa kwa kutumia sampuli lengwa.

Katika uteuzi wa washiriki, wanafunzi walichaguliwa kwa kuzingatia kiwango chao cha ufaulu na uwezo wao wa kujieleza kwa Kiswahili ili kupata mitazamo tofauti kuhusu mikakati ya ujifunzaji. Hatimaye, data zote zilizokusanywa zilipangwa na kuchambuliwa kimaelezo kwa kuzingatia mada zilizojitokeza kuhusu mikakati ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Uchambuzi huu uliwezesha kubaini mikakati inayotumika kwa vitendo na mchango wake katika kuboresha ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili katika shule teule wilayani Musanze

**Mikakati Iliyobainika**

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa walimu na wanafunzi hutumia mikakati mbalimbali ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika

ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Mikakati iliyobainika ni pamoja na uboreshaji wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, ushirikiano baina ya walimu wa Kiswahili, matumizi ya teknolojia mbadala, mashindano na mijadala katika lugha ya Kiswahili, pamoja na uhamasishaji wa wanafunzi kujifunza Kiswahili. Mikakati hii inajadiliwa kwa kina hapa chini kwa kuzingatia data za ushuhudiaji na usaili, huku Nadharia ya Viwezeshi ikitumiwa kuendesha mjadala

**Kuboresha Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji**

Matumizi ya makundi ya wanafunzi ni mkakati mkuu unaotumika na walimu wa Kiswahili katika shule teule wilayani Musanze kukabiliana na changamoto ya uhaba wa vitabu na kamusi, huku mkakati huo ukikuza ushirikiano na mwingiliano wa lugha miongoni mwa wanafunzi. Ufundishaji ni mchakato wa mwalimu kupitisha maarifa na stadi kwa wanafunzi kwa kutumia mbinu mbalimbali, huku ujifunzaji ni mchakato wa mwanafunzi kupokea na kujenga maarifa hayo kupitia uzoefu na mwingiliano na mazingira ya kielimu (Rivers, 1981). Katika muktadha wa Kiswahili kama lugha ya pili, mbinu za ufundishaji zinazoshirikisha wanafunzi kwa vitendo ni muhimu kwa sababu zinakuza matumizi halisi ya lugha (Dörnyei, 2001). Data za ushuhudiaji zilibainisha kuwa walimu hushirikisha wanafunzi katika makundi ili idadi ya vitabu vichache iendane na makundi. Kuhusu suala la kamusi, ilibidi mwanafunzi asimame aende kwenye meza ya mwalimu kutafuta maana ya neno analotaka kwa kuwa kamusi ni moja tu. Data za usaili zinashadidia matokeo haya kupitia Mwalimu wa Kiswahili kutoka shule ya A ambaye anaeleza:

> Mimi, kama mwalimu, huunda makundi ya wanafunzi ili kuhakikisha ushiriki wa kila mmoja wao katika somo. Kila kundi hupewa kitabu kimoja au viwili kulingana na mahitaji ili kuwezesha wanafunzi wote kuelewa vizuri

> maudhui ya somo. Kwa kutumia njia hii, ninawahusisha wanafunzi wote kikamilifu katika mchakato wa ujifunzaji. Njia hii inaniwezesha kufikia malengo ya somo kama yalivyopangwa.

Dondoo hili linaonesha kuwa mbinu ya kutumia makundi inarahisisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Mwalimu huchagua mbinu hii ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa vitabu ambavyo havitoshelezi mahitaji ya shule. Nadharia ya Viwezeshi inatubainishia kuwa vitabu na kamusi ni viwezeshi vya kimwili vinavyowezesha ujifunzaji wa lugha (Gibson, 1977). Pale viwezeshi hivi vinapokuwa vichache, walimu hulazimika kuunda viwezeshi vya kijamii kama vile makundi ya wanafunzi ili kuziba pengo hilo.

Matokeo haya yanaonesha kwamba walimu si wapokeaji tu wa viwezeshi vilivyopo, bali ni waundaji wa viwezeshi vipya wanapokabiliana na changamoto za rasilimali (Ndikubwimana, 2023). Mtazamo huu unaendana na hoja za Zhong (2024) anayeeleza kuwa upangaji wa wanafunzi katika makundi ni mkakati wa ufundishaji unaowezesha usimamizi bora wa darasa lenye wanafunzi wengi na kuongeza muda wa wanafunzi kutumia lugha kwa vitendo ndani ya kipindi kifupi cha somo. Aidha, Shani (2019) anabainisha kuwa walimu katika stadi ya kusoma hufanya jitihada za kuunda makundi madogo ya wanafunzi ili kuhakikisha kila mwanafunzi anashiriki kikamilifu, huku wanafunzi wenye ujuzi zaidi wakisaidia wenzao kuelewa maneno magumu.

Hivyo, matumizi ya makundi katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya pili wilayani Musanze yanaonekana kuwa kiwezeshi cha kijamii kinachosaidia kupunguza athari za ukosefu wa viwezeshi vya kimwili. Hali hii inathibitishwa na mhimili wa viwezeshi vya kijamii wa Nadharia ya

Viwezeshi ambao unasisitiza kwamba mwingiliano baina ya wanafunzi unaweza kuwa chanzo muhimu cha ujifunzaji (Gibson, 1977). Vilevile, usaili kati ya mtafiti na mwalimu unafanana na matokeo ya ushuhudiaji kwa kuwa, katika mchakato huo, ilibainika kuwa matumizi ya makundi yanawapa wanafunzi fursa ya kushiriki kikamilifu kwa kutoa mawazo yao binafsi. Pia, makundi huimarisha ushirikiano miongoni mwa wanafunzi katika kujifunza Kiswahili. Kwa mujibu wa Niyomugabo (2016), serikali inapaswa kuongeza idadi ya vitabu vinavyogawiwa kwa shule za umma. Iwapo serikali itatoa vitabu na kamusi kwa wingi na kwa aina mbalimbali, changamoto ya uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia haitajitokeza tena.

**Kuimarisha Ushirikiano Baina ya Walimu**

Ushirikiano baina ya walimu wa Kiswahili kupitia makundi ya mitandao ya kijamii ni mkakati muhimu unaowasaidia walimu kubadilishana maarifa, uzoefu, na mbinu za kufundishia, na hivyo kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa semina rasmi za kitaaluma. Ushirikiano katika ufundishaji ni mchakato wa walimu kushirikiana na kubadilishana maarifa, uzoefu, na mbinu za kufundishia ili kuboresha utendaji wao (Şahin, 2023). Data za usaili na walimu wa Kiswahili zilibainisha kuwa walimu wanashirikiana wao kwa wao kupitia makundi ya mitandao ya kijamii kama vile *WhatsApp*. Kushirikiana kwao kunawaongeza ujuzi na weledi katika lugha ya Kiswahili. Jambo hili linathibitishwa na mwalimu wa Kiswahili wa shule B kwa kusema:

> Kwa kweli, sisi kama walimu wa Kiswahili, tunashirikiana bega kwa bega ili tuwe na fununu kwa kila chochote katika Kiswahili. Tunashirikiana na wenzetu kwa kuelewa kinachofaa au kisichofaa. Tuna makundi yanayotuhusisha walimu wa Kiswahili. Ninapofeli

> kuelewa kitu fulani, ninajaribu kuwauliza wenzangu ili wanisaidie.

Dondoo hili linaonesha kwamba walimu hutumia makundi ya mitandao ya kijamii kama kiwezeshi cha kijamii na kitaaluma katika kuboresha ujuzi wao wa Kiswahili. Kulingana na Nadharia ya Viwezeshi, ushirikiano huu unawakilisha kiwezeshi cha kijamii, ambapo walimu huunda mazingira wezeshi kwa njia ya kubadilishana maarifa na uzoefu (Gibson, 1977). Pale ambapo mwalimu anakosa ufahamu wa jambo fulani katika Kiswahili, wenzake katika kundi la mitandao ya kijamii huwa kiwezeshi cha kupata jibu na kuendelea na ufundishaji wake kwa ufanisi.

Kulingana na Şahin (2023), ushirikiano wa walimu katika elimu ya lugha ni jambo muhimu katika kuboresha ubora wa ufundishaji na maendeleo ya kitaaluma. Anabainisha kwamba vitendo vya ushirikiano (kama vile upangaji wa masomo wa pamoja, uchunguzi wa rika, usanifu wa nyenzo za pamoja, na ushiriki katika jumuiya za kitaaluma za kujifunza) huimarisha utendaji wa kutafakari na ufanisi wa ufundishaji kwa walimu. Anaongeza kuwa ushirikiano huwaongezea walimu uwajibikaji wa pamoja na kujenga utamaduni wa ujifunzaji endelevu.

Ili kuwa na maendeleo katika elimu, ni lazima wanaohusika wakuze na kumwendeleza mwalimu katika mchakato wake wa ufundishaji. Walimu ambao bado wapo kazini ni lazima wapewe semina kuhusu mbinu za kisasa zinazoendana na ufundishaji (Kafu, 2007; Mbito, 2013). Miima na Kawoya (2021) wanabainisha kuwa kutayarisha warsha maalumu mara kwa mara kwa walimu wa shule za upili kuhusu mbinu za ufundishaji za kisasa kutafanikisha umilisi wa walimu katika mchakato wa ufundishaji wa Kiswahili. Hivyo basi, matokeo ya utafiti huu yanashadidia hoja za

wataalamu hawa kwa kuonesha kwamba walimu wa Kiswahili wilayani Musanze wanajiendeleza kupitia ushirikiano wa mitandao ya kijamii kutokana na ukosefu wa semina rasmi; na kwamba, serikali haina budi kuwaandalia walimu warsha na semina kuhusu mbinu za kisasa za ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya pili.

**Kutumia Teknolojia Mbadala katika Ufundishaji wa Kiswahili**

Walimu wa Kiswahili katika shule teule wilayani Musanze hutumia simu zao za mkononi kama teknolojia mbadala ya kufundishia, hasa kurekodi nyimbo na sauti za Kiswahili ili kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa vifaa vya kiteknolojia shuleni. Matumizi ya teknolojia ni kiwezeshi muhimu katika ufundishaji wa lugha ya pili. Hoja hii inathibitishwa na Mwalimu wa Kiswahili wa shule A kwa kusema:

> Mimi ninaandaa somo kabla ya wakati, ikiwa ni nyimbo, ni lazima nizirekodi kabla ya kufundisha. Ninatumia simu yangu kwa kuwa hapa shuleni hatuna vifaa vya ujifunzaji vya kiteknolojia. Walimu hatuna tarakilishi zinazotosha, redio wala televisheni. Kwa hiyo, ninatumia simu yangu ili somo liendelee.

Dondoo hili linaonesha kuwa walimu hutafuta njia yoyote ile ili kufanikisha malengo ya ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Kwa mtazamo wa Nadharia ya Viwezeshi, simu ya mkononi ya mwalimu inakuwa kiwezeshi cha kimwili (ambacho ni mhimili mmojawapo wa nadharia hii) kinachobadilisha nafasi ya maabara ya lugha na vifaa vingine vya kiteknolojia visivyopatikana (Gibson, 1977).

Fikra iliyomo katika dondoo la Mwalimu wa Kiswahili wa shule A inashadidiwa na Odera (2007) ambaye anabainisha kuwa sauti zilizorekodiwa husaidia katika kazi za kurudia, kwani hujenga uzoefu wa

lugha usiopatikana kwa urahisi kupitia mwalimu pekee. Upatikanaji wa vifaa vya teknolojia kama redio, tarakilishi, na televisheni hurahisisha na kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Matumizi ya teknolojia huongeza uelewa, motisha, na umilisi wa lugha kwa wanafunzi (Niyomugabo, 2016; Vicent na Msigwa, 2021).

Kwa ujumla, matokeo ya sehemu hii yanaonesha kwamba ingawa viwezeshi vya kimwili kama vile maabara na tarakilishi havipo katika shule teule wilayani Musanze, walimu wameunda viwezeshi mbadala kwa kutumia simu zao za mkononi. Hali hii inaafikiana na Nadharia ya Viwezeshi inayosema kwamba mazingira yenye vikwazo bado yanaweza kutoa fursa za kujifunza endapo wahusika wataunda viwezeshi vipya (Gibson, 1979).

**Kuandaa Mashindano ya Lugha ya Kiswahili**

Mashindano ya mijadala na midahalo ya Kiswahili ni mikakati inayotumiwa na walimu ili kuboresha ujuzi wa mazungumzo. Pia, hutumika kujenga ujasiri wa kuongea hadharani kwa wanafunzi wenye uwezo finyu wa lugha. Data za ushuhudiaji zilionesha kuwa walimu huwapa wanafunzi mada tofauti za kuzungumzia na kufanya mijadala baina yao. Data za usaili zinashadidia matokeo haya kupitia Mwalimu wa Kiswahili wa shule ya B ambaye anaeleza:

> Sisi walimu wa Kiswahili tunashirikisha wanafunzi katika mashindano ya Kiswahili. Tunawashirikisha katika mijadala na midahalo ya Kiswahili kwa kuwapa mada tofauti. Mada hizo zinawafanya kutafuta msamiati wa kutumia wakati wa kuwasilisha kazi hizo. Mashindano hayo yanawaongezea nguvu za kuongea na kurudia yale yaliyosemwa hadharani.

Dondoo hili linaeleza kuwa walimu wanatumia mijadala na midahalo ili kuboresha mazungumzo na uwezo finyu wa lugha kwa wanafunzi. Kwa mtazamo wa Nadharia ya Viwezeshi, mashindano ni viwezeshi vya kijamii vinavyounda mazingira ya kutumia lugha kwa vitendo (Gibson, 1977). Kupitia mhimili wa viwezeshi vya kisaikolojia wa Nadharia ya Viwezeshi, tulibaini kuwa mashindano haya hujenga kujiamini na kuwapa motisha wanafunzi, mambo ambayo ni muhimu katika ujifunzaji wa lugha ya pili.

Niyomugabo (2016) anaunga mkono matokeo haya kwa kueleza kuwa, ili kuwahamasisha wanafunzi, ni vema shule zitayarishe mashindano kuhusu lugha ya Kiswahili. Anasisitiza kuwa wanafunzi waelekezwe namna ya kuandika nyimbo, mashairi na tamthilia. Mashindano ya aina hii huwasaidia kujitetea, kujitambulisha, pamoja na kukuza vipaji vyao katika lugha ya Kiswahili. Miima na Kawoya (2021) wanashadidia hoja hii kwa kusema kuwa kuandaa mashindano ya mara kwa mara ya umilisi katika lugha ya Kiswahili na kuwatuza washindi huweza kukuza mazungumzo katika Kiswahili.

**Kuwamotisha Wanafunzi**

Uhamasishaji wa wanafunzi kuhusu umuhimu wa Kiswahili katika fursa za ajira, biashara, na mawasiliano ya kikanda ni mkakati wa kisaikolojia unaotumiwa na walimu kujenga motisha na mtazamo chanya wa wanafunzi kuelekea lugha hiyo, licha ya kutokuwepo kwake katika mitihani ya taifa. Motisha ni nguzo muhimu katika ujifunzaji wa lugha ya pili (Dörnyei, 2001). Data za ushuhudiaji zinaonesha kuwa walimu hutembelea kila kundi la wanafunzi ili kubaini changamoto walizonazo na kuwafafanulia pale inapobidi. Data za usaili zinashadidia matokeo haya kupitia Mwalimu wa Kiswahili kutoka shule A ambaye anaeleza:

> Mimi, kama mwalimu wa Kiswahili, ninawahamasisha wanafunzi na kuwaelezea umuhimu wa lugha ya Kiswahili. Ninawaambia wanafunzi kuwa lugha ni muhimu sana katika maisha yao ya kila siku. Wanafunzi wasipinge Kiswahili kwa kuwa huenda baada ya kesho lugha hii inaweza ikawasaidia katika kupata ajira, biashara, na mawasiliano ya kikanda.

Dondoo hili linaonesha kuwa walimu hutumia uhamasishaji kama njia ya kujenga motisha kwa wanafunzi. Nadharia ya Viwezeshi ilituongoza kubaini kuwa uhamasishaji huu unawakilisha kiwezeshi cha kisaikolojia, ambapo mwalimu huunda mtazamo chanya wa mwanafunzi kuelekea lugha (Gibson, 1977). Pale mwanafunzi anapoelewa kuwa Kiswahili kina thamani katika maisha yake ya sasa na ya baadaye, motisha yake ya kujifunza huongezeka.

Kiswahili kina nafasi ya kuwasaidia, kuwaunganisha na kuwatambulisha wanafunzi katika ushirikiano wa kikanda na maendeleo ya Afrika Mashariki (Mukuthuria, 2006). Matokeo haya yanashadidiwa na Zhong (2024) ambaye anabainisha kuwa mikakati ya kufundisha inapoendana na malengo, mahitaji ya mawasiliano ya maisha halisi, na mambo yanayovutia, wanafunzi huonesha motisha ya ndani na kushiriki kikamilifu katika kazi za darasani. Aidha, Jarvis (2005), Harrison (2004) na Maina (2003) wanabainisha kuwa motisha huimarika pale wanafunzi wanapopata maoni chanya, kushirikishwa katika shughuli za darasani, na kuhisi kuwa lugha wanayojifunza ina thamani. Mutheu (2019) anaongeza kuwa ushirikishwaji wa wazazi na utamaduni wa kusoma unaweza kuhamasisha wanafunzi na kuboresha matokeo ya ujifunzaji wa Kiswahili.

Kwa ujumla, kumtia moyo mwanafunzi kujifunza ni hatua muhimu katika utekelezaji wa mtaala (Filgona na wenzake, 2020) kwa sababu motisha ni

jambo lenye ushawishi mkubwa katika hali za ufundishaji na ujifunzaji. Hatimaye, mafanikio ya ujifunzaji yanategemea ikiwa wanafunzi wamehamasishwa au la, kwani motisha huwasukuma kufikia malengo ya kujifunza.

**Hitimisho**

Utafiti uliozalisha makala hii ulichunguza mikakati inayotumika kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili katika shule za upili nchini Rwanda. Mtafiti alitumia mbinu za ushuhudiaji na usaili ili kupata uelewa kuhusu hali halisi ya ufundishaji wa Kiswahili katika shule teule wilayani Musanze. Data zilizokusanywa zilichambuliwa kwa njia ya kimaelezo ili kufafanua kwa undani mikakati iliyopo katika mazingira halisi ya ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya pili.

Makala imebainisha mikakati mitano inayotumika. Mkakati wa kwanza ni kuboresha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kupitia uundaji wa makundi ya wanafunzi. Mkakati huu husaidia kukabiliana na uhaba wa vitabu na kamusi, huku ukikuza ushirikiano na mwingiliano wa lugha. Mkakati wa pili ni kuwapo kwa ushirikiano baina ya walimu kupitia mitandao ya kijamii. Mkakati huu huwaongezea walimu ujuzi na weledi katika kufundisha. Mkakati wa tatu ni kutumia simu za mkononi kwa ajili ya kurekodi nyimbo na sauti za Kiswahili. Mkakati huu huwasaidia wanafunzi kuiga matamshi sahihi. Mkakati wa nne ni kuandaa mashindano ya Kiswahili. Mkakati huu huongeza matumizi ya lugha na kujenga ujasiri wa kuongea hadharani. Mkakati wa tano ni kuhamasisha wanafunzi kuhusu umuhimu wa Kiswahili katika fursa za ajira na biashara hujenga mtazamo chanya na motisha ya kujifunza.

Kwa ujumla, matokeo haya yaliyochagizwa na Nadharia ya Viwezeshi ya Gibson (1977) yanathibitisha kwamba mazingira ya shule na ubunifu wa walimu vina mchango mkubwa katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Ingawa viwezeshi vya kimwili kama vile vitabu, kamusi na maabara ni vichache, walimu wamefanikiwa kubadilisha mazingira hayo duni kuwa wezeshi kwa kutumia viwezeshi vya kijamii kama vile ushirikiano, makundi na mijadala, pamoja na viwezeshi vya kisaikolojia kama vile motisha na uhamasishaji. Hivyo, kwa kuwa mafanikio ya ujifunzaji yanategemea mchanganyiko wa viwezeshi mbalimbali, ni vema walimu wanaofundisha Kiswahili kama lugha ya pili wakatumia viwezeshi ili kurahisisha ujifunzaji.

**Marejeleo**

Akaka, L. (2017). Changamoto Zinazowakabili Walimu katika Ufundishaji wa Kiswahili katika Shule za Upili Nchini Kenya. *Kioo cha Lugha*, 11 (1), 47-57.

Cary, S. (2000). *Working with Second Language Learners: Answers to Teachers' Top Ten Questions*. Portsmouth: Heinemann.

Crystal, D. (1997). *English as a Global Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

Dörnyei, Z. (2001). *Motivational Strategies in the Language Classroom*. Cambridge: Cambridge University Press.

Filgona, J., Sakiyo, J., Gwany, D. M. na Okoronka, A. U. (2020). Motivation in Learning. *Asian Journal of Education and Social Studies*, 10(4), 16-37. Inapatikana katika https://doi.org/10.9734/ajess/2020/v10i430273. Ilisomwa tarehe 21 Januari 2026.

Gathumbi, A. W. na Masembe, S. C. (2005). *Principles and Techniques in Language Teaching: A Text for Teacher Educators, Teachers and Pre-Service Teachers*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Gibson, J. J. (1977). The Theory of Affordances. Katika R. Shaw na J. Bransford (Wah.), *Perceiving, Acting, and Knowing: Toward an Ecological Psychology* (kur. 67-82). Hillsdale: Lawrence Erlbaum Associates.

Gibson, J. J. (1979). *The Ecological Approach to Visual Perception*. Boston: Houghton Mifflin.

Harrison, C. (2004). *Understanding Reading Development*. London: Sage Publications.

Jarvis, M. (2005). *The Psychology of Effective Teaching and Learning*. Cheltenham: Nelson Thornes.

Kafu, P. A. (2007). Challenges of Teacher Education in the 21st Century: The Kenyan Experience. *The Educator*, *1*, 9-16.

Maina, E. N. (2003). *An Investigation into the Causes of Poor Performance in Kiswahili KCSE Examination in Kipipiri Division of Nyandarua District* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Mbito, J. (2013). *Challenges Facing Teachers and Students in the Process of Teaching and Learning Kiswahili in Public Secondary Schools in Kiambu District in Kiambu County, Kenya* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi

Miima, F.A. na Kawoya, V. F. (2021). Mstakabala na Changamoto za Kiswahili Nchini Uganda. East *African Journal of Swahili Studies*, 3(1), 70-77.

Mlaga, W. K. (2017). Historia ya Kiswahili Nchini Rwanda: Kielelezo cha Utashi wa Kisiasa katika Ustawi wa Lugha ya Kiswahili. *Kioo cha*

*Lugha*, *15*, 1-19. Inapatikana katika https://www.ajol.info/index.php/kcl/article/view/16289. Ilisomwa tarehe 17 Septemba 2023.

Mukuthuria, M. (2006). Kiswahili and Its Expanding Roles of Development in East African Cooperation: A Case of Uganda. *Nordic Journal of African Studies*, *15*(2), 154-165.

Mutheu, W.A. (2019). *An Assessment of Challenges and Strategies in Teaching and Learning of Kiswahili in Public Secondary Schools in Hamisi Sub-County* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Maseno, Kenya.

Ndikubwimana, F. (2023). *Changamoto za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Pili nchini Rwanda. Mfano wa Shule Teule Wilayani Musanze* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Rwanda, Rwanda.

Niyomugabo, C. (2016). Ufundishaji wa Kiswahili katika Shule za Rwanda: Historia, Tathmini ya Makosa, Matatizo na Mahitaji. *Kiswahili*, 79 (1), 78-92.

Ntawiyanga, S. (2020). Makosa ya Upatanishi wa Kisarufi katika Ujifunzaji Lugha ya Pili: Mfano wa Wanafunzi wa Kiswahili katika Shule za Upili Wilayani Muhanga, Nchini Rwanda. *Kioo cha Lugha*, 17(1), 15-32. Inapatikana katika https://doi.org/10.4314/kcl.v17i1. Ilisomwa tarehe 16 Septemba 2023.

Odera, F. (2007). Learning Kiswahili Language by Radio at Distance in Secondary Schools in Nyakach, Nyando District, Kenya. *Malaysian Journal of Education*, 9(2), 89-106.

Oloo, M. A. (2018). *Masuala Yanayoathiri Ufunzaji na Ujifunzaji wa Somo la Ufahamu katika Shule za Upili katika Kaunti ya Kisumu nchini Kenya* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro, Kenya.

Rivers, W. M. (1981). *Teaching Foreign Language Skills* (toleo la 2). Chicago: University of Chicago Press.

Rwanda Education Board (REB). (2015). *Muhtasari wa Somo la Kiswahili: Kidato cha 4-6, Michepuo ya Lugha*. Kigali: Rwanda Education Board.

Şahin, İ. (2023). Teacher Collaboration in English Language Teaching (ELT) Research: A Systematic Review. *Melius: Journal of Narrative and Language Studies*, 1(1), 58-90. Inapatikana katika https://dergipark.org.tr/en/pub/melius/issue/78152/1252549. Ilisomwa tarehe 17 Julai 2023.

Saleh, H.F. (2019). *Changamoto za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni katika darasa Mseto la Wingilugha,* (Tasnifu ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Zanzibar.

Shani, S.K. (2019). *Changamoto Zinazowakabili Walimu Katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni katika Stadi ya Kusoma* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Zanzibar.

Vicent, S. na Msigwa, A. B. G. (2021). Umuhimu na Changamoto za TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili kwa Wageni. *Mulika*, 40 (2), 142-157.

Yang, H. (2008). On Teaching Strategies in Second Language Acquisition. *US-China Education Review*, 5 (1), 61-67.

Zhong, Y. (2024). Research on Teaching Strategies Based on Second Language Acquisition Theory. *Communications in Humanities Research,* 51, 108-113. Inapatikana katika https://doi.org/10.54254/2753-7064/51/20242526. Ilisomwa tarehe 24 Februari 2026.